Utdannings-
direktoratet

# MFUMO WA ELIMU WA NORWEI

## KUANZIA WATOTO WACHANGA HADI VIJANA

Taarifa kwa wazazi na walezi wapya waliofika



UU

udir.no

## YALIYOMO

Elimu ya watoto wachanga na malezi (umri wa miaka 0–6) Katika lugha ya kinorwei: barnehage ..... 3

Elimu ya msingi na sekondari ya chini (umri wa miaka 6-16) katika lugha ya kinorwei: grunnskole ..... 3

- Haki na wajibu wa kuhudhuria shule ya msingi na sekondari ya chini ..... 4
- Majaribio ya mitihani na kupeana alama ..... 4
- Programu za kabla na baada ya shule (katika lugha ya kinorwei: SFO) ..... 4

Elimu ya juu ya sekondari kwa vijana (umri wa miaka 16-24) katika lugha ya kinorwei: videregående opplæring ..... 4

- Kutuma ombi katika shule ya juu ya sekondari ..... 5
- Programu za masomo ya jumla (katika lugha ya Kinorwei: studieforberedende utdanningsprogram) ..... 5
- Programu za elimu ya kiufundi (katika lugha ya Kinorwei: yrkesfaglige utdanningsprogram) ..... 5

Haki za wanafunzi wote ..... 6

- Mafunzo maalum ya lugha ..... 6
- Msaada wa utangulizi katika shule za msingi, sekondari za chini na sekondari za juu ..... 6
- Elimu maalum ..... 7
- Mazingira salama na chanya ya masomo ..... 7
- Ushirikiano kati ya shule na nyumbani ..... 7

## ELIMU YA WATOTO WACHANGA NA MALEZI (UMRI WA MIAKA 0–6) KATIKA LUGHA YA KINORWEI: BARNEHAGE

Watoto wengi nchini Norwei huhudhuria elimu na malezi ya utotoni, ambayo mara nyingi hujulikana kama chekechea, hadi wanapoanza shule wanapofikisha umri wa miaka 6.

Katika shule ya chekechea watoto hutunzwa na wafanyakazi wenye ujuzi ambao huwaelekeza katika masomo, kucheza na shughuli mbalimbali za kijamii na kitamaduni. Katika shule ya chekechea watoto hukaa kwa muda wakiwa ndani na nje ya darasa. Chekechea ni muhimu katika kukuza lugha ya watoto, maendeleo ya kijamii na kimwili.

Ni muhimu kuwa na ushirikiano na mazungumzo kati ya wazazi au walezi na shule ya chekechea. Shule ya chekechea itahitaji taarifa kuhusu historia ya mtoto, kama vile lugha asilia na lugha zingine zinazozungumzwa, maslahi na changamoto zinazowezekana, ili kukidhi mahitaji ya mtoto kwa ufanisi. Shule ya chekechea pia itatoa taarifa kwa wazazi/walezi kuhusu shughuli za kila siku na ukuaji wa mtoto.

Katika shule ya chekechea, watoto wote wana haki ya kuwa na mazingira salama na yenye afya. Shule ya chekechea inakuza jamii jumuishi na inazuia kudhulumiwa na tabia zingine hatari. Ikiwa mtoto atadhulumiwa au kuwekwa katika tabia zingine hatari na watoto wengine au watu wazima, shule ya chekechea ina wajibu wa kuchukua hatua na kukabiliana na hali hiyo.

Watoto walio na mahitaji maalum wanaweza kuwa na haki ya msaada maalum wa kielimu na mwongozo. Hii pia inatumika kwa watoto ambao hawajaandikishwa katika shule ya chekechea. Msaada unaotolewa unaendana na mahitaji ya mtoto.

Kuna shule za chekechea za umma na za kibinafsi. Unaweza kuwasiliana na manispaa yako kwa maelezo zaidi kuhusu haki, kutuma maombi, ada ya mzazi na chaguo zilizopo katika jamii yako.

## ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI YA CHINI (UMRI WA MIAKA 6-16) KATIKA LUGHA YA KINORWEI: GRUNNSKOLE

Watoto na vijana wenye umri wa miaka 6-16 wana haki na wajibu wa kuhudhuria elimu ya msingi na sekondari ya chini. Manispaa inatoa elimu ya msingi kwa umma na sekondari ya chini bila malipo na inapatikana kwa watoto wote. Shule za kibinafsi kwa kawaida hutoza ada.

Kwa kawaida watoto huanza shule wanapofikisha umri wa miaka 6. Shule ya msingi huchukua miaka saba kuanzia gredi ya 1 hadi ya 7. Shule ya sekondari ya chini huchukua miaka tatu, kuanzia gredi ya 8 hadi ya 10.

Mwaka wa shule kwa kawaida huanza katikati ya mwezi Agosti na kumalizika katikati ya mwezi Juni. Watoto na vijana wanaofika Norwai mwaka wa shule unapoendelea, wataandikishwa shuleni haraka iwezekanavyo.

**Haki na wajibu wa kuhudhuria shule ya msingi na sekondari ya chini**
Watoto na vijana wanaowasili Norwaei wana haki ya kuhudhuria shule za msingi na za sekondari ya chini ikiwa kuna uwezekano kwamba watakaa nchini kwa zaidi ya miezi mitatu. Manispaa inalazimika kuandikisha mtoto shuleni haraka iwezekanavyo na sio zaidi ya mwezi mmoja baada ya kuwasili nchini.

Baada yawatoto na vijana kuishi Norwei kwa miezi mitatu, wana wajibu wa kuhudhuria shule ya msingi ya umma au shule ya sekondari ya chini au taasisi ya elimu anapofaa kuwa.

**Majaribio ya mitihani na kupeana alama**
Katika shule ya msingi, wanafunzi hupokea majaribio ya mitihani bila kupewa alama. Katika shule ya sekondari ya chini, wanafunzi hupokea majaribio ya mitihani pamoja na alama na bila kupewa alama.

Gredi kutoka shule ya sekondari ya chini hutumiwa wakati wanafunzi wanaomba nafasi katika shule ya sekondari ya juu. Kiwango cha gredi kinaanzia 1 hadi 6, huku 6 ikiwa gredi ya juu zaidi inayoweza kufikiwa.

**Programu za kabla na baada ya shule (katika lugha ya kinorwei: SFO)**
SFO hutolewa kabla na baada ya shule na huwezesha michezo na shughuli za kitamaduni na burudani chini ya usimamizi wa wafanyakazi waliohitimu. SFO mara nyingi hufanyika ndani au karibu na majengo ya shule.

Manispaa nyingi hutoa SFO kwa watoto wote katika gredi ya 1-4 na kwa watoto wenye mahitaji maalum katika gredi ya 1-7.

Programu za kabla na baada ya shule huwezesha michezo, masomo na shughuli mbalimbali za kijamii na kitamaduni kulingana na umri wa watoto na kiwango chao cha utendaji. Programu hii hukuza hali ya umiliki na urafiki, na ni muhimu kwa ukuaji wa watoto katika hali ya kijamii, kitamaduni na lugha.

Kushiriki katika programu za kabla na baada ya shule ni kwa hiari. Unaweza kuwasiliana na manispaa yako kwa maelezo zaidi kuhusu kuhudhuria SFO na ada ya mzazi.

## ELIMU YA JUU YA SEKONDARI KWA VIJANA (UMRI WA MIAKA 16-24) KATIKA LUGHA YA KINORWEI: VIDEREGÅENDE OPPLÆRING

Vijana ambao wamemaliza shule ya sekondari ya chini nchini Norwe au elimu linganisho katika nchi nyingine, wana haki ya kupata elimu ya sekondari ya juu.

Hii inatumika pia kwa wale ambao wamemaliza elimu ya juu ya sekondari katika nchi nyingine ambayo haitambuliwi kama cheti cha jumla cha kujiunga na chuo na chuo kikuu nchini Norwei au kufuzu katika ufundi stadi.

Wanafunzi wengi hujiunga na shule ya juu ya sekondari wanapofikisha umri wa miaka 16. Watu wazima wanaotuma ombi (umri wa miaka 25 na zaidi) wanaweza kuwa na haki ya kupata elimu ya juu ya sekondari iliyoandaliwa hasa kwa ajili ya watu wazima.

Haki ya kujiandikisha katika shule ya juu ya sekondari, inahitaji ukaaji halali kisheria nchini Norwei. Vijana wanaokaa nchini maombi yao ya kupata kibali cha kuishi yanapohughulikiwa, wana haki ya kupata elimu ya juu ya sekondari wakiwa na umri wa chini ya miaka 18, na kuna uwezekano kwamba watakaa nchini kwa zaidi ya miezi mitatu. Vijana wanaokaa nchini wakisubiri kibali cha ukaaji kuamuliwa na wanaofikisha umri wa miaka 18 mwakani, wana haki ya kumaliza mwaka wa masomo.

**Kutuma ombi katika shule ya juu ya sekondari**
Elimu ya juu ya sekondari imegawanywa katika programu za masomo ya jumla na elimu ya kiufundi. Mwaka wa kwanza unajulikana kama “vg1” na mwombaji huonyesha mapendekezo matatu ya kwanza ya programu tofauti na ana haki ya kukubaliwa katika mojawapo. Mwanafunzi atalazimika kutuma ombi kwa kila mwaka (vg1, vg2 na vg3).

Kama sheria, vijana hutuma ombi kwa shule ya juu ya sekondari katika kaunti wanayoishi. Mamlaka za kaunti zinawajibika kutoa elimu ya juu ya sekondari ya umma bila malipo. Pia kuna shule za kibinafsi ambazo kwa kawaida hutoza ada.

Tarehe ya mwisho ya kutuma ombi la kujiunga na shule ya juu ya sekondari ni tarehe 1 Februari au 1 Machi kila mwaka. Tarehe ya mwisho ya kutuma ombi ya tarehe 1 Februari inawahusu wanafunzi ambao wamewasili nchini Norwei hivi majuzi, ambao hawana alama za shule ya chini ya sekondari kwa sababu ya mafunzo maalum ya lugha au wana haki ya kutathminiwa kibinafsi kuhusiana na maombi yao.

Kwa maelezo zaidi kuhusu elimu ya juu ya sekondari, mchakato wa kutuma maombi na uandikishaji, tafadhali wasiliana na mamlaka ya kaunti yako au nenda kwenye www.vilbli.no, ambayo inatoa habari katika lugha mbalimbali.

**Programu za masomo ya jumla (katika lugha ya Kinorwei: studieforberedende utdanningsprogram)**
Programu za masomo ya jumla hutoa cheti cha jumla au maalum cha uandikishaji katika chuo na chuo kikuu. Gredi kutoka shule ya juu ya sekondari hutumiwa wakati wanafunzi wanatuma ombi la elimu ya juu katika vyuo na vyuo vikuu.

Programu za masomo ya jumla zina muda wa kawaida wa miaka mitatu ya masomo.

Watu wanaotuma maombi wanaweza kuchagua kati ya programu zifuatazo za masomo ya jumla:

- Utaalam katika masomo ya jumla
- Sanaa, muundo na usanifu (Art, design and architecture)
- Spoti na elimu ya kimwili (Sports and physical education)
- Muziki, ngoma na maigizo (Music, dance and drama)
- Vyombo vya habari na mawasiliano (Media and communication)

**Programu za elimu ya kiufundi (katika lugha ya Kinorwei: yrkesfaglige utdanningsprogram)**
Programu za elimu ya ufundi stadi hutoa sifa ya ufundi stadi, ikiwa na au bila cheti cha biashara au cheti cha msafiri. Sifa ya ufundi stadi humpa mtu sifa za kufanya mazoezi ya taaluma.

Programu za elimu ya ufundi stadi zina muda wa kawaida wa miaka mitatu ya mafundisho ya darasani au miaka miwili ya mafundisho ya darasani na miaka miwili ya mafunzo katika kampuni. Pia inawezekana kujiandikisha katika programu ya ziada ya cheti cha jumla cha chuo na chuo kikuu.

Watu wanotuma maombi wanaweza kuchagua kati ya programu zifuatazo za elimu ya ufundi stadi:

- Ujenzi na utengenezaji (Building and construction)
- Uhandisi wa umeme na teknolojia ya kompyuta (Electrical engineering and computer technology)
- Ususi, upangaji maua, muundo wa ndani na rejareja (Hairdresser, floral, interior and retail design)
- Afya, ukuzaji wa watoto na vijana (Healthcare, childhood and youth development)
- Ufundi, muundo na uundaji wa bidhaa (Crafts, design and product development)
- Teknolojia ya habari na uzaliji wa habari (Information technology and media production)
- Kilimo, uvuvi na utunzaji misitu (Agriculture, fishing and forestry)
- Mkahawa na usindikaji wa chakula (Restaurant and food processing)
- Uuzaji, huduma na utalii (Sales, service and tourism)
- Uzalishaji wa kiteknolojia na viwanda (Technological and industrial production)

## HAKI ZA WANAFUNZI WOTE

Haki hizi zinatumika kwa wanafunzi wa shule za msingi, sekondari za chini na sekondari za juu.

**Mafunzo maalum ya lugha**
Wanafunzi wenye lugha ya mama zaidi ya Kinorwei au Kisami, ambao hawazungumzi Kinorwei au walio na ujuzi duni wa lugha ya Kinorwei, wana haki ya kupata mafunzo maalum ya lugha. Haki inatumika hadi lugha yao ya Kinorwei iwe bora vya kutosha ili waweze kuhudhuria na kufaidika na elimu ya kawaida.

Mafunzo maalum ya lugha yanajumuisha mafunzo ya ziada katika lugha ya Kinorwei, na yanaweza pia kujumuisha:

- Maelekezo katika lugha ya mama ya mwanafunzi
- Elimu katika lugha mbili - ambayo inachanganya mafundisho katika somo moja au zaidi katika lugha ya Kinorwei na lugha ambayo mwanafunzi anaifahamu.

Shule inahitajika kutathmini ujuzi wa mwanafunzi katika lugha ya Kinorwei ili kubaini ni aina gani ya elimu ya lugha maalum inafaa kwa mwanafunzi.

**Msaada wa utangulizi katika shule za msingi, sekondari za chini na sekondari za juu**
Watoto na vijana ambao wamewasili nchini Norway hivi majuzi, wanaweza kupokea elimu yote au sehemu yake katika vikundi, madarasa au shule tofauti kwa kipindi cha hadi miaka miwili. Kusudi ni kujifunza lugha ya Kinorwei haraka, kabla ya kuingia shule au madarasa ya kawaida.

Mtoto au kijana na wazazi au walezi wake, wanapaswa kufahamishwa vyema kuhusu maudhui ya programu ya utangulizi, na idhini ya kuingia katika programu hiyo. Mtoto au kijana na wazazi au walezi wake, wanaweza kuchagua badala yake kuingia shule au madarasa ya kawaida.

**Elimu maalum**

Wanafunzi ambao hawana au hawawezi kufaidika vya kutosha kutokana na elimu ya kawaida, wanaweza kuwa na haki ya elimu maalum. Elimu maalum inaweza kumaanisha kuwa mwanafunzi anafanyia kazi malengo ya kujifunza mwenyewe, kwamba mwalimu au msaidizi anafuatilia na kumsaidia mwanafunzi darasani au kwamba mwanafunzi anapewa vifaa maalum. Elimu maalum inatolewa kulingana na mahitaji maalum ya mwanafunzi.

**Mazingira salama na chanya ya masomo**

Wanafunzi wote wana haki ya kuwa na mazingira salama na chanya ya masomo ambayo yanakuza afya njema, ustawi na masomo. Ni uzoefu wa mwanafunzi mwenyewe wa mazingira ya shule ambao ni muhimu. Wanafunzi wote wanapaswa kuhisi wanahusika. Ni jukumu la shule kuzuia unyanyasaji na tabia zingine hatari. Shule inahitajika kufuatilia hali na kutekeleza hatua ikiwa mwanafunzi hajisikii kuwa salama au mzima shuleni.

**Ushirikiano kati ya shule na nyumbani**

Ushirikiano kati ya shule, mwanafunzi na wazazi au walezi ni muhimu. Hii husaidia shule kumsaidia vyema mwanafunzi na huchangia katika ukuaji mzuri wa kielimu na kijamii.

Wazazi au walezi wana wajibu wa kuhudhuria mazungumzo ya maendeleo baina ya shule na mtoto, na mikutano ya wazazi kwa wazazi wote katika darasa au kikundi ambacho mtoto anahusika.

Wazazi au walezi wanakaribishwa kila mara kuwasiliana na shule wakiwa na maswali au maswala yoyote kuhusu elimu na ukuaji wa mtoto wao.

Utdannings-
direktoratet

udir.no